**BODI YA USAJILI WA WABUNIFU MAJENGO NA WAKADIRIAJI MAJENZI (AQRB)**
(Chini ya Sheria Na. 4 of 2010)

# TAARIFA KWA UMMA

## ONYO KWA KAMPUNI AU MTU BINAFSI KUJIHUSISHA NA KAZI AU MAJUKUMU YA UBUNIFU MAJENGO NA UKADIRIAJI MAJENZI PASIPO KUSAJILIWA NA BODI

Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB) inatoa ONYO KALI kwa watu wanaochora na kuuza ramani/michoro ya Ubunifu Majengo na kusambaza katika VITABU, MAJARIDA katika maeneo ya BARABARA, MITANDAO YA JAMII kama FACEBOOK, INSTAGRAM N.K Dar es Salaam na mikoa yote Tanzania Bara.

Aidha, Bodi inatoa TAHADHARI kwa wananchi wote kutonunua au kutumia Michoro hiyo ambayo imebuniwa na watu wasiosajiliwa na kutambulika kisheria. Hivyo kuuza au/ na kutumia michoro hiyo ni kinyume na sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi Na.4 ya mwaka 2010 bali pia kunaweza kuleta madhara katika matumizi yake kwani wanaochora hawajasajiliwa na Bodi na hivyo Viwango na Usalama wa ramani au michoro hiyo haufahamiki ama kuwa chini ya viwango.

Ikumbukwe kuwa michoro yoyote ya ujenzi hufanywa na wataalamu waliosomea fani hizo na wana sifa zakusajiliwa kisheria ili kuhakikisha kazi zao zinafuata maadili ya taaluma na kukidhi viwango vya ujenzi wa jengo husika, kwa kuzingatia matumizi mbalimbali na aina ya eneo husika. Si kila ramani ya jengo inafaa katika kila eneo la ujenzi kwani kila eneo la ujenzi lina mazingira tofauti kama vile hali ya hewa, miundo mbinu iliyopo, miteremko, aina ya udongo, matumizi ya jengo n.k. Kwa maana hiyo tunasisitiza katika uchoraji wa jengo wananchi washirikishe Wataalamu waliosajiliwa watakaoweza kubuni michoro inayoendana na mahitaji ya eneo husika.

Aidha, Bodi inawataka watu wote wanaojihusisha na KUCHORA na KUUZA RAMANI ZA MAJENGO KINYUME NA SHERIA KUACHA MARA MOJA, na endapo watakaidi onyo hili, BODI itawachukulia hatua za kisheria chini ya sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriji Majenzi Na. 4/ 2010.

**IMETOLEWA NA MSAJILI**
**BODI YA USAJILI WA**
**WABUNIFU MAJENGO NA WAKADIRIAJI MAJENZI (AQRB)**